JARIDA LA

# Mkoa wa Dodoma

*Fahari ya Watanzania*

www.dodoma.go.tz Toleo la 0014






**Ipeleke Dodoma Duniani, Ilete Dunia Dodoma**

MHARIRI
Francisca F. Mselemu

SAFU YA WACHANGIAJI
Francisca F. Mselemu
Hellen M. Minja
Happiness E. Chindiye
Stephano H. Silaa

MSANIFU JARIDA
Stephano H. Silaa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

# Salamu za Mkuu wa Mkoa



Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kinara wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira



**Mhe. Rosemary Senyamule**
**Mkuu wa Mkoa wa Dodoma**

Napenda kuwakaribisha kusoma toleo la mwezi Februari la jarida la Mkoa wa Dodoma, linaloendelea kuhabarisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali na maendeleo ya Mkoa wetu.

Katika mwezi huu, Ofisi yangu iliendelea kusimamia vikao muhimu vya kuboresha huduma kwa wananchi, ikiwemo kikao na Maafisa Ardhi na Mazingira, ambapo niliwasisitiza kufanya kazi kwa weledi, uadilifu na kuwajibika ipasavyo, kwa kuzingatia hadhi ya Dodoma kama Makao Makuu ya Nchi.

Tuliendelea pia kuimarisha uhifadhi wa mazingira kupitia mpango wa kupanda miche ya miti milioni 1.5 kwa kila Halmashauri, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kukabiliana na uharibifu wa misitu.

Aidha, tulifanya tathmini ya utekelezaji wa Mkataba wa Lishe, ambapo Halmashauri zilitakiwa kuhakikisha utoaji wa fedha za lishe kwa wakati. Utekelezaji umefikia asilimia 95, hatua inayotia moyo, huku jitihada zaidi zikihitajika katika maeneo yenye changamoto, hususan upatikanaji wa maji.

Vilevile, maazimio mbalimbali yalifikiwa ili kuboresha hali ya lishe, ikiwa ni pamoja na kuongeza vituo vya huduma kwa watoto wenye utapiamlo na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali.

Natoa wito kwa Watumishi wa Umma, wadau na Wananchi kuendelea kushirikiana katika kuleta maendeleo ya Mkoa wetu.

Mwisho, nawahakikishia kuwa tutaendelea kusimamia maendeleo ya Dodoma kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.

Mungu ibariki Dodoma,

Mungu ibariki Tanzania.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

# Maoni ya Mhariri



**FRANCISCA F. MSELEMU**

**Kaimu Mkuu Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma**

Katika juhudi za kuijenga jamii yenye afya bora na yenye uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo, suala la lishe bora linabaki kuwa nguzo muhimu isiyoweza kupuuzwa. Lishe bora si tu msingi wa afya njema kwa mtu mmoja mmoja, bali pia ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa taifa kwa ujumla.

Ni ukweli usiopingika kuwa jamii yenye lishe duni hukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo udumavu kwa watoto, kupungua kwa nguvu kazi, na kuongezeka kwa magonjwa yanayoweza kuzuilika. Hali hii huathiri moja kwa moja tija ya uzalishaji na ustawi wa jamii. Hivyo basi, uwekezaji katika lishe bora ni uwekezaji katika rasilimali `watu.

Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuonesha dhamira thabiti ya kuboresha hali ya lishe nchini kupitia utekelezaji wa mikakati na programu mbalimbali za lishe. Miongoni mwa juhudi hizo ni kuimarisha utekelezaji wa Mkataba wa Lishe katika ngazi zote za utawala, kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu umuhimu wa mlo kamili na bora, pamoja na kuhamasisha uzalishaji na matumizi ya vyakula vyenye virutubisho muhimu.

Aidha, ushirikiano kati ya Serikali, wadau wa maendeleo, sekta binafsi na jamii kwa ujumla umeendelea kupewa kipaumbele katika kupambana na changamoto za lishe. Ni kupitia mshikamano huu ndipo mafanikio ya kudumu yanaweza kupatikana, hususan katika kuhakikisha watoto, akina mama na makundi mengine yaliyo hatarini wanapata lishe stahiki.

Ni wajibu wa kila mmoja wetu kuchukua hatua kwa nafasi yake, kuanzia ngazi ya familia hadi jamii, katika kuhakikisha tunazingatia kanuni za lishe bora. Elimu ya lishe inapaswa kupewa nafasi katika malezi ya watoto, na matumizi ya vyakula vya asili vinavyopatikana katika mazingira yetu yahamasishwe zaidi.

Jarida hili linatoa wito kwa wadau wote kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuimarisha hali ya lishe Nchini. Kwa pamoja, tunaweza kujenga jamii yenye afya bora, yenye nguvu kazi imara, na yenye uwezo wa kufikia malengo ya maendeleo endelevu.



## SERIKALI YASHAURIWA KUANDAA MPANGO WA KUPANDA MITI KATA KWA KATA

Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Pinda, ameishauri Serikali kuandaa Mpango wa kupanda miti Kata kwa Kata kwa kuwatumia vijana ambao ni nguvu kazi ya Taifa ili kutimiza azma ya kulinda na kuhifadhi mazingira kwa matokeo bora ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mhe. Pinda ameyasema hayo alipokua akiongoza zoezi la upandaji miti lililoandaliwa na Taasisi ya Habari Conservation Organization (HCO) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) kwenye eneo la Chimwanga, Njedengwa Jijini Dodoma lenye ukubwa wa Ekari 72 leo Februari 06, 2026 zoezi ambalo pia limehudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule.

“Tukichukua watendaji wa Kata na Mitaa, tunaweza ‘ku-organize’ vijana hawa na kazi ikawa nzuri tukiifanya kuwa ‘event’ ya kila mwaka, kila tunapopata miti ya kutosha, tunahama kutoka Kata hizi tunakwenda Kata zinazofuata, kwa sababu suala la umwagiliaji sio tatizo kwa miti 20 au 40 kwenye mstari mmoja, maji yapo, na mimi nipo tayari kuwa Championi wa hilo jambo”.

Aidha, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule, amesema Mkoa wake umeendelea na Kampeni mbalimbali za upandaji miti na kwa sasa kampeni inayoendelea ni upandaji wa miti ya matunda ili kuwapa motisha wananchi kupata faida za kivuli, chakula na uchumi hali inayoongeza mwamko wa kupanda miti hususan mti wa tunda la Tufaa.

Nae, Mwenyekiti wa Taasisi ya Habari Conservation Organization (HCO) Bi. Loyce Joseph, amesema miti ni fagio la Mungu linalotumika kusafisha hewa ukaa na kuzalisha hewa safi kwani mazingira yanapoharibiwa, athari zake ni mateso hivyo, miti inayopandwa inatarajiwa kunufaisha watu wote bila upendeleo na kutengeneza mandhari nzuri ya Jiji la Dodoma.



## MACHINGA JIJINI DODOMA KUJENGEWA SOKO LA KUDUMU UMONGA

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, Februari 06, 2026, amefanya ziara fupi ya ukaguzi wa eneo litakalojengwa soko kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo maarufu kama Machinga wa Jiji la Dodoma lililopo katika eneo la Umonga Jijini humu.

Katika ziara hiyo fupi, Mhe. Dkt. Nchemba ameipongeza Halmashauri ya Jiji kwa kutenga eneo hilo kwani lipo katikati ya Mji na ni eneo la makazi ya watu huku akisisitiza miundombinu ya soko hilo iwe ya kisasa kulingana na eneo lilipo soko hilo

"Rais wetu alishaelekeza bajeti ijayo huwenda kukawa na 5% ambayo itahusika na miundombinu tu, matarajio yetu kwa kuwa hili soko lipo mjini liwe na mazingira nadhifu sio zizi la ngombe, hili ni soko la kisasa kuanzia mtu anapoingia mpaka anapofanya biashara, miundombinu ya kisasa, liwe safi linalovutia mtu atamani kufika hapa kila mara, kila mtu afanye kazi kwenye mazingira safi".

Akiwasilisha mpango wa ujenzi wa soko hilo, Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma Dkt. Frederick Sagamiko, amesema eneo hilo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 8,621 linatarajiwa kujengwa Soko la kudumu litakalochukua wafanyabiashara waliokua kwenye soko la Rehema Nchimbi, na litakuwa na miundombinu na huduma zote muhimu ikiwa ni pamoja na kituo cha Mabasi ya abiria.







## MAAFISA UGANI WAPATIWA MAFUNZO KUTAMBUA VIWANGO ENDELEVU VYA UZALISHAJI MAZAO YA KIMKAKATI

Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) Kanda ya Kati, imetoa mafunzo ya siku moja kwa Maafisa Ugani 80 wa ngazi za Kata na Vijiji kutoka Halmashauri nane za Mkoa wa Dodoma yakilenga katika kuwajengea uwezo wa kutambua viwango endelevu vya uzalishaji wenye tija kwa mazao ya kimkakati yanayolimwa katika Mkoa wa Dodoma.

Akifungua mafunzo hayo yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Jijini hapa, Februari 06, 2026, Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Dkt. Khatibu Kazungu, ameainisha malengo mahsusi ya mafunzo hayo;

“Malengo mahsusi ya mafunzo haya ni kuwajengea uwezo ninyi kuhusu viwango na miongozo ya mazao ya Mbaazi, Choroko, Soya na Ufuta, kujiwekea mikakati bora ya kuwahudumia wakulima katika mazao ya kimkakati lakini pia kuratibu mpango kazi wa mafunzo kwa wakulima, wakulima viongozi na utekelezaji wa majukumu katika maeneo yao ya kazi katika msimu huu”.

Akizungumzia matarajio baada ya mafunzo hayo, Mkuu wa Kanda ya Kati (COPRA) Bw. Andrew F. Mgaya amesema wanatarajia Maafisa Ugani hao kwenda kutoa elimu kwa wakulima wa ngazi za Kata na Vijiji ili waweze kuzalisha kwa tija kutokana na Mamlaka yake kutoa mbegu za Mbaazi tani 2.5 hivi karibuni kwa Mkoa huu hivyo wanahitaji usimamizi mzuri na matokeo yenye tija.





## VIONGOZI WA SERIKALI NGAZI ZOTE WANA WAJIBU WA KUSIMAMIA UTUNZAJI WA MAZINGIRA

Dodoma, Februari 08, 2026 Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, amezindua kampeni ya upandaji miti katika Kata ya Iyumbu, iliyoandaliwa na Umoja wa Wananume wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika Mteule wa Iyumbu Jijini Dodoma na kutoa msisitizo juu ya suala la utunzaji wa mazingira kuwa ni wajibu wa viongozi wa ngazi zote.

Mhe. Senyamule amesema, utunzaji wa mazingira unahitaji usimamizi wa karibu wa Viongozi wa Serikali katika ngazi husika kuanzia Vijiji, Kata, Wilaya, Mkoa hadi Taifa kwa ujumla huku akitoa msisitizo juu ya kuzingatia sheria ya kuzuia mifugo kuzurura ovyo mitaani kwnai inachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira.

“Tusimamie wajibu wa utunzaji wa mazingira katika maeneo yetu ili Makao Makuu ya nchi iendane na unadhifu wa mazingira yake, lakini pia niagize viongozi wa Serikali ngazi hizi, mifugo inayotembea au kuchungwa, sheria ya Serikali kwa mijini inasema, ufugaji sio wa kutembeza mifugo barabarani, ni kuiweka ndani na kuihudumia kwa chakula.

Aidha, Mchungaji Kiongozi wa Kanisa hilo Naftaly Njawike, amesema utunzaji wa mazingira ni agizo la Mungu na Kiongozi Mkuu wa Kanisa hilo hivyo, ni wajibu wa Kanisa kushirikiana na Serikali katika utunzaji wa mazingira sambamba na kuwalea wananchi kiroho kwa kuwasisitiza juu ya umuhimu wa mazingira ambayo ndio chanzo cha uhai wa mwanadamu.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanaume KKKT Usharika Mteule wa Iyumbu Bw. Ernest Mcharo, amesema wamejiwekea lengo la kupanda miti 3,000 ndani ya kipindi cha miezi mitatu (Januari – Machi) ambapo mpaka sasa wameshapanda miti 2,420 katika kaya 484 za Kata hiyo na kila kaya imepanda wastani wa miti mitano na kampeni yao imebebwa na kauli mbiu ya ‘Iyumbu ya Kijani, inaanza na nyumba yangu’






## RC SENYAMULE AUKARIBISHA UMIKIDO, AUTAKA KUWA CHACHU YA MAWASILIANO KATI YA SERIKALI NA WANANCHI

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, ameukaribisha Umoja wa Vyombo vya Habari vya Mitandao ya Kijamii Mkoa wa Dodoma (UMIKIDO) na kuutaka kuwa chachu ya kuimarisha mawasiliano kati ya Serikali na wananchi kupitia utoaji sahihi wa taarifa pamoja na ubunifu wa maudhui.

Mhe. Senyamule ametoa kauli hiyo Februari 9, 2026, mara baada ya viongozi wa UMIKIDO kufika ofisini kwake kwa lengo la kujitambulisha na kuomba ushirikiano na Serikali ya Mkoa wa Dodoma.

“Hongereni kwa kuanzisha umoja huu. Nimefurahishwa sana kwani utarahisisha kazi na kuwa kiunganishi muhimu kati ya Serikali ya Mkoa na vyombo vya habari vya mitandaoni. Tulitamani kupata watu wanaozungumza lugha moja na Serikali, na tunaamini ninyi ni wazalendo,” amesema Mhe. Senyamule.

Ameeleza kuwa uwepo wa umoja huo utaisaidia Serikali kufikisha taarifa kwa wananchi kwa ufanisi zaidi, sambamba na kuongeza uelewa wa Umma kuhusu shughuli na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

“Ni muhimu Watanzania wakaendelea kufahamu kazi zinazofanywa na Serikali. Nina imani mtakuwa wabunifu katika kuandaa na kusambaza taarifa kwa njia zitakazowafikia wananchi kwa urahisi” ameongeza.

Aidha, Mhe. Senyamule amewataka wanachama wa UMIKIDO kuzingatia kutangaza miradi ya kimkakati na mipango ya maendeleo, ikiwemo uhifadhi wa mazingira, matumizi ya nishati safi ya kupikia, sekta ya utalii na michezo, pamoja na kuhamasisha matukio mbalimbali kuelekea mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027.

Awali, viongozi wa UMIKIDO walieleza dhamira na malengo ya kuanzishwa kwa umoja huo, ikiwa ni pamoja na kuimarisha maadili ya uandishi wa habari za mitandaoni na kushirikiana kwa karibu na Serikali katika utoaji wa taarifa sahihi kwa Umma. Pia waliomba ushirikiano kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ili kutimiza malengo hayo.



## CRDB BANK FOUNDATION WATAMBULISHA 'IMBEJU' KUWEZESHA WANAWAKE WAJASIRIAMALI

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, ambaye pia ni muasisi wa mpango wa Wanawake na Samia unaolenga kuwakomboa wanawake kiuchumi, ameishukuru Taasisi ya CRDB Bank Foundation kwa juhudi zake endelevu za uwezeshaji wa wanawake wajasiriamali mkoani Dodoma. Shukrani hizo zilitolewa katika kikao maalum na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Esther Mwambapa, kilicholenga kuimarisha ushirikiano katika kukuza uchumi wa wanawake kupitia mpango huo.

Katika mazungumzo hayo, Mwambapa alimweleza Mkuu wa Mkoa kuwa CRDB Bank Foundation imetenga shilingi bilioni 2 kwa ajili ya kuwawezesha wanawake wajasiriamali waliopo katika mpango wa Wanawake na Samia kote nchini. Alifafanua kuwa uwezeshaji huo utafanyika kwa utaratibu maalum unaojumuisha mafunzo ya elimu ya fedha, usimamizi wa biashara na ufuatiliaji wa karibu, ili kuhakikisha wanawake wanatumia mitaji hiyo kukuza biashara zao kwa ufanisi na kwa matokeo endelevu.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa alitoa wito kwa wanawake kutumia fedha hizo kwa nidhamu na malengo sahihi, akisisitiza kuwa Serikali inatamani kuona wanawake wakipiga hatua kubwa kiuchumi.

Ameipongeza CRDB Bank Foundation kwa kazi nzuri inayoifanya kupitia mikopo ya asilimia 10 na kuisifu programu ya IMBEJU akisema imekuwa chachu muhimu katika kuchochea maendeleo na kuibua fursa mpya kwa wanawake nchini.








## MKANDARASI SOKO LA MAJENGO ATAKIWA KUTENGENEZA MPANGO MKAKATI WA UKAMILISHAJI WA MRADI

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, amewataka Wakandarasi na Mshauri wa Serikali wanaosimamia Mradi wa ujenzi wa soko la Majengo Jijini Dodoma, kutengeneza mpango kazi utakaoonesha namna mradi huo utakavyoweza kukamilika kwa wakati uliowekwa ambao ni tarehe 05, Machi, 2026.

Maelekezo hayo yametolewa wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi huo yanayokwenda sambamba na utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na Waziri Mkuu wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba alipofanya ziara katika soko hilo Desemba 12, 2025 juu ya Mradi huo kukamilika kwa wakati.

“Nawapa kazi hapa Wakandarasi, hebu ‘mu-establish’ huu mpangilio hapa, ‘Consaltant’, kwa kazi hii, ili iishe tarehe 5 mnatakiwa mfanye nini, maana tunachosema siku zote kwa mafundi wengine, ni kazi zifanyike tofauti lakini kwa wakati mmoja kwa zile ambazo zinaweza kufanyika pamoja lakini bado huyu ambaye ni mtaalam kabisa, anafanya kazi moja akimaliza ndio anakwenda nyingine”. Mhe. Senyamule.

Kadhalika, Mkandarasi Msimamizi wa Mradi Masalu Kifutumo, ameomba kuongezewa muda wa kukamilika kwa mradi kwani mpaka sasa umefikia 44.5% ingawa mahitaji ya kukamilisha mradi yapo ya kutosha na mengine yameagizwa hivyo, yakifika kwa wakati, wana uhakika mradi utakamilika kama unavyotarajiwa.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa Mradi huo, Mhandisi Mshauri wa Serikali Prosper Shayo, amesema kusuasua kwa mradi huo kunatokana na changamoto ya rasilimali watu ambayo si toshelevu, vifaa vya ujenzi na mitambo kuchelewa kufika eneo la Mradi na wamemshauri Mkandarasi kuongeza nguvu na endapo atafanya hivyo, Mradi utakamilika sio chini ya siku 60.







## KANISA KATOLIKI DODOMA LAADHIMISHA UTAKATIFU WA VINCENZA MARIA PALONI WA VERONA

Kanisa Katoliki Jimbo Kuu Mkoa wa Dodoma, limeadhimisha Misa takatifu ya shukrani ya kufuatia kutangazwa Mtakatifu Sista Vincenza Maria Piloni ambaye ni mwanzilishi wa Shirika la Masista wa Misericordia wa Verona Italia ibada ambayo imeadhimishwa na Mhashamu Beatus Kinyaiya, Askofu Mkuu wa Jimbo hilo Februari 14, 2026.

Misa hiyo imehudhuriwa na wageni mbalimbali pamoja na Viongozi wa Serikali, wakiwemo Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Pinda na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule sambamba na viongozi wa Kanisa hilo kutoka Majimbo ya mikoa tofauti tofauti Nchini.

Akizungumza baada ya Misa hiyo, Mhe. Senyamule amezungumzia umuhimu wa kuacha alama ya upendo kwa kutumia mfano wa Mtakatifu huyo kwani licha ya kufariki dunia miaka mingi iliyopita, bado anaendelea kukumbukwa kwa matendo yake ya upendo.

"Wote tujikumbushe kuwa kumbe kuishi ni kuacha alama, Sista Vincenza ameacha alama ambapo amefariki miaka mingi iliyopita lakini leo tunaendelea kumtaja na kumuenzi kwa matendo yake makuu, tumekua tukiambiwa kila siku tuishi kwa kuacha alama kwenye maisha yetu na huyu ameacha alama kubwa, akizungumzia upendo".

Mtakatifu Vincenza Maria Paloni alizaliwa Januari 26, 1802 nchini Italia ambapo kwa miaka mingi ya maisha yake, alijishughulisha na matendo ya huruma na upendo, alifariki Novemba 11, 1855 ambapo kutokana na utumishi wake wa kuwahudumia wahitaji, unyenyekevu na upendo, alitangazwa kuwa Mtakatifu shujaa wa upendo na Papa Leo XIV mwaka 2025 Roma, Italia.









## WAZALISHAJI WA MVINYO MKOA WA DODOMA KUPATA SOKO LA UHAKIKA NCHINI BURUNDI

Balozi wa Tanzania nchini Burundi Mhe. Gelasius G. Byakanwa, amefanya kikao na wazalishaji na wachakataji wa zao la Zabibu wanaozalisha Mvinyo (Wine) Mkoa wa Dodoma akilenga kutangaza bidhaa hiyo nchini Burundi ambayo ni ya kipekee kuzalishwa nchini Tanzania katika Mkoa wa Dodoma Februari 16,2026.

Kikao hicho kimefanyika katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Jengo la Mkapa Jijini hapa ambapo Mhe. Balozi Byakanwa amesema anaandaa maonesho ya Mvinyo unaozalishwa Dodoma nchini Burundi mwezi Mei, 2026, ambapo wachakataji hao watapata fursa ya kutangaza soko lao nchini humo.

“Moja ya malengo tuliyojiwekea mwaka huu kwenye ofisi yetu ni kutaka kutangaza bidhaa za Mvinyo kwenye soko la Burundi, tukijifungia sisi wenyewe ofisini hatuzalishi Wine, tutabaki na malengo, tukaona ipo haja ya kuja kukutana na wazalishaji, tuwahoji kama mpo tayari kwenda Burundi kutangaza bidhaa zenu? Mkisema ndio, sisi tunapiga hatua ya pili ya malengo yetu”.

Aidha, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule, amepongeza jitihada za Balozi huyo kutangaza soko la Mvinyo nchini Burundi na kusema kuwa hatua hiyo itakwenda kumaliza kabisa changamoto ya upatikanaji wa soko la zabibu hususan kinywaji adhimu cha Mvinyo kwani Dodoma imekua na uzalishaji mkubwa lakini soko ndio limekua si la uhakika.

“Mwaka 2022, tulikua na viwanda vitatu tu vya kuchakata zabibu, tulipata changamoto kubwa ya soko, jambo lile lilileta tafakuri ya namna gani tunaweza kusaidia wakulima hawa Zabibu zao zisiozee shambani na badala yake waanze kuuza kwa hatua ya kuchakata, hiyo ndio ilifanya mabadiliko haya tunayoyaona leo hapa tuna viwanda zaidi ya 40 katika miaka hii mitatu ya changamoto”.

Nao, baadhi ya wachakataji na wazalishaji wa mvinyo, wamefurahia fursa hiyo na kumhakikishia Balozi kwamba watashiriki maonesho hayo na kusema kuwa watajitahidi kuzalisha bidhaa zenye ubora na viwango vya kimataifa kwani wazo lake limekuja wakati sahihi kwa muktadha wa zao la zabibu na mvinyo ni Fahari ya Dodoma, hivyo linapaswa kutangazwa kwa maslahi ya nchi nzima.



## WAKURUGENZI WAELEKEZWA KUTOA FEDHA ZA LISHE KWA WAKATI KWANI SIO HIARI

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, amewaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri za Mkoa wa Dodoma kutoa fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa afua za lishe hususan ile ya kutoa fedha shilingi 1000 kwa kila mtoto.

Mhe. Senyamule aliyasema hayo wakati akifungua kikao cha kutathmini utekelezaji wa mkataba wa lishe kwa nusu mwaka (Julai – Desemba 2025) kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa ofisi yake, jengo la Mkapa Jijini Dodoma kilichowahusisha Wajumbe wa kamati ya lishe Ngazi ya Mkoa, Wakuu wa Wilaya,Wakurugenzi,Maafisa Lishe, Maafisa Elimu Sekondari, Maafisa Elimu Msingi wa Halmashauri zote za Mkoa wa Dodoma sambamba na Wadau mbalimbali wa lishe.

“Hawa watoto wakiwa na udumavu watakuja kulisumbua Taifa, ukifikiria kwa upana, utaitoa fedha ya lishe kabla ya fedha nyingine yeyote kwa sababu utafikiria hili unalolifanya lina athari chanya kwa nchi lakini ukilifikiria kwa udogo, huwenda ukaona ni jambo rahisi sana kutotoa fedha za lishe. Niendelee kusisitiza suala la kutoa fedha za lishe,shilingi 1000 kwa kila mtoto ni wajibu na sio hiari”

Kadhalika, taarifa ya utekelezaji wa viashiria vya lishe iliyowasilishwa na Afisa Lishe Mkoa wa Dodoma Bi. Herriet Carin, imeonesha kuwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa afua za lishe katika kipindi hiki, zimetolewa kwa 95%, ingawa kiwango cha utekelezaji ni 54% hivyo, kasi inahitajika zaidi ili kufikia lengo la 100% kwa Mkoa ifikapo Juni 2026.

Akitoa maoni yake juu ya kuimarisha lishe shuleni, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa Mhe. Mayeka S. Mayeka, alisema kuwa kama Mkoa, kuna haja ya kuweka Mpango Mkakati wa kuchimba visima kwenye shule za msingi ili kuwa na uhakika wa maji ya kumwagilia bustani kwani moja ya changamoto zilizowasilishwa ni bustani nyingi za mbogamboga kufa kutokana na kukosekana maji ya kumwagilia.

Kikao hicho kilifikia maazimio kadhaa ikiwemo kuongeza vituo vya huduma kwa watoto wenye utapiamlo mkali, kiandaliwe kikao cha Wataalam wa lishe na viongozi wa madhehebu ya dini, ubunifu uwepo wa namna ya kuendeleza chakula cha lishe mchanganyiko kwa kutoa elimu juu ya uchakataji wa chakula hasa kipindi hiki cha mvua ili vyakula vya mbogamboga viweze kutumika kipindi cha kiangazi.



## WATAALAM WA ARDHI NA MAZINGIRA WATAKIWA KUWA NA DHAMIRA MOJA YA KUITUNZA MAKAO MAKUU DODOMA

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, amefanya kikao na Wataalam wa sekta za ardhi na mazingira kilicholenga kuwakumbusha wajibu wao kwenye utoaji wa huduma kwa wananchi huku akiwasisitiza kuwa na dhamira moja ya kutoa huduma bora kwa Wananchi sambamba na kuitunza makao makuu ya nchi kwani uwezo wa kufanya hivyo wanao.

Akizungumza na Maafisa hao wakati wa kikao kilichofanyika kwenye ukumbi wa ofisi yake jengo la Mkapa Jijini hapa, Mhe. Senyamule alisema suala la kuwatumikia wananchi si la hiari kwani wote wana utaalam ndio maana wamepewa dhamana hiyo hivyo wasipofanya kazi katika viwango vinavyohitajika, itaonesha kuwa wamekosa dhamira katika utumishi wao.

"Watanzania wenzetu wakija Makao Makuu na kuona tumeweza kuitunza vizuri, ina miti inapendeza, kila mtu atafurahi kuwa Makao Makuu yetu ni nzuri kwa hiyo tuliopewa dhamana hizi, sekta ya ardhi na mazingira, nimesisitiza na kuamini kuwa mmenielewa, nisipoona mabadiliko nitaamini sasa watu wamekosa dhamira lakini sababu ya kufanya hivyo tunayo, uwezo wa kufanya hivyo tunao kwa sababu wote tuna utaalam kwa kazi tulizopewa lakini tuna dhamana tuliyopewa, kwa hiyo mtu asipofanya kazi hiyo, amekosa dhamira"

Katika kikao hicho pia iliwasilishwa taarifa ya Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) ambayo imeeleza kuwa katika kuhifadhi mazingira, TFS imeweka lengo kupanda miche ya miti 1,500,000 kwa kila Halmashauri ili kurudisha misitu inayopotea kila mwaka ambayo ni takribani hekta laki 4 hadi 5 kutokana na sababu mbalimbali za kilimo, mifugo na ukataji miti kwa ajili ya nishati.

Kikao hicho kilifikia maazimio kadhaa ikiwa ni pamoja na; Halmashauri ziwezeshwe na Wizara ya ardhi katika uandaaji wa matumizi bora ya ardhi, kufanyika kikao kazi kati ya Jiji la Dodoma na Halmashauri ya Chamwino kwa ajili ya kuhuisha mpango kabambe kwa Jiji la Dodoma kwenye maeneo ya kiutawala, Mamlaka za Serikali za mitaa kuandaa maeneo mahsusi kwa ajili ya upandaji miti na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi zinazosimamia uhifadhi wa mazingira kudhibiti shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya hifadhi ya Bonde la Mzakwe na mengine ndani ya Mkoa.






# BANDARI KAVU YA IHUMWA JIJINI DODOMA YAANZA SHUGHULI ZA UCHUKUZI KWA MIZIGO YA NDANI YA NCHI

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, Februari 20, 2026, amefanya ziara ya kikazi kukagua eneo la Bandari kavu lililopo Ihumwa Jijini Dodoma ambapo amefurahishwa na hatua zilizochukuliwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Wizara ya Uchukuzi ambazo ni utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwamba, Treni ya abiria ya mwendo kasi itakapoanza usafirishaji na ile ya kusafirisha mizigo ianze mara moja.

Mhe. Senyamule amesema, Bandari hiyo imeanza usafirishaji wa mizigo ya ndani ya nchi ambayo inatokea Pugu Jijini Dar es salaam mpaka eneo hilo la Bandari kavu ambapo hatua hiyo imeongeza fursa za kiuchumi kwa wakazi wa Jiji la Dodoma kutokana na kuongezeka kwa shughuli mbalimbali za uchukuzi katika eneo hilo ambapo takribani watu 300 hadi 500 hufanya kazi hapo kwa siku.

“Kwetu Mkoa hii ni fursa kubwa ambayo itachechua uchumi wa wananchi kwani magari yanakuja kutoka sehemu mbalimbali kushusha na kupakia mizigo, lakini kikubwa zaidi ni matarajio tuliyonayo sasa kama ambavyo wenzetu wa Bandari wanavyotuahidi kuwa kipande cha kukamilisha reli kuingia baharini ili kuanza kupakia mizigo kipo hatua za mwisho za ukamilishaji, jambo hilo tunalisubiri kwa hamu”.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania, Afisa Mipango Mwandamizi Bw. Innocent Kapinga, amesema mradi huo umeanzishwa kwa malengo mahsusi ya kupunguza gharama za usafirishaji na kuongeza ufanisi wa mnyororo wa usafirishaji, kurahisisha upokeaji wa mizigo, kupunguza msongamano Bandarini na kuifanya Dodoma kuwa kitovu cha kibiashara kwa usafirishaji wa mizigo.

Aidha, Mkurugenzi wa Michezo kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Bw. Yussuph Singo, amesema Michezo, Sanaa na Utamaduni vimepewa kipaumbele katika kufikia malengo ya Dira 2050 na ni kati ya mambo ambayo yatahitajika kuinua kipato cha Mtanzania kufikia kwenye dola 7000 hivyo, kuanzisha kituo hicho kikubwa cha michezo kitasaidia kufikia malengo ya Taifa.



## BALOZI WA TANZANIA NCHINI BURUNDI ATEMBELEA KIWANDA CHA ALKO VINTAGE

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary S. Senyamule, amewaagiza wataalamu wa RUWASA Wilaya ya Chemba kufanya tathmini ya eneo jirani na mradi wa maji ili wananchi wanaoathirika wapatiwe fidia stahiki.

Maelekezo hayo ameyatoa leo Februari 19, 2026, akiwa katika eneo la mradi huo wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo wilayani Chemba. Mhe. Senyamule amesisitiza umuhimu wa kulinda vyanzo vya maji huku haki za wananchi zikizingatiwa.

"Ninatoa maelekezo kwa RUWASA mfanye tathmini ya kina ili kubaini wananchi wanaostahili kufidiwa, lengo likiwa kulinda chanzo hiki muhimu cha maji pamoja na maslahi ya wananchi," amesema Mhe. Senyamule.

Akitoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa, Mhandisi wa Maji wa RUWASA Chemba, Deogratius Kambarage, amesema zaidi ya shilingi bilioni 11 zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji unaotarajiwa kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa wilaya hiyo.

Aidha, katika ziara hiyo, Mhe. Senyamule alikagua ujenzi wa Shule ya Msingi Chemba iliyopo Tarafa ya Goima na kupongeza maendeleo ya ujenzi wa shule mpya unaogharimu shilingi 397,200,000/=. Kukamilika kwa mradi huo kunatarajiwa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi, walimu na jamii kwa ujumla.

Mbali na mradi wa maji na shule, Mkuu wa Mkoa pia alikagua miradi mingine ikiwemo kilimo cha tufaa katika shamba darasa lenye miche 400, ujenzi wa nyumba za watumishi katika Hospitali ya Wilaya ya Chemba pamoja na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.

"Serikali itaendelea kusimamia miradi ya maendeleo ili kuhakikisha thamani ya fedha inaonekana na wananchi wanapata huduma bora zinazochochea ustawi wa kijamii na kiuchumi," ameongeza Mhe. Senyamule.





## WAZIRI AKWILAPO ATOA MAELEKEZO KUMALIZA MGOGORO WA ARDHI MAHOMANYIKA, DODOMA

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo, Februari 25, 2026, amekutana na wakazi wa eneo la Mahomanyika lililopo katika Kata ya Nzuguni 'A' Jijini Dodoma kwa lengo la kutoa maelekezo yatakayomaliza mgogoro wa ardhi uliodumu kwa muda mrefu bila kupatiwa ufumbuzi.

Maelekezo hayo ni pamoja na kupangwa na kupimwa kwa eneo hilo ambalo ni la Serikali, kwa ajili ya utatuzi wa migogoro iliyopo pamoja na matumizi ya Serikali, kipaumbele cha upangaji huo kiwe ni kutatua changamoto za wananchi wa Jiji la Dodoma ambao wamekua wakidai viwanja kwa muda mrefu, viwanja 352 vilivyoingizwa na Jiji kwenye mfumo wa Tausi kwa ajili ya kuuzwa viendelee lakini visiingizwe viwanja vipya.

Aidha, ameongeza kuwa eneo litakalobaki lipangwe na kupimwa kwa madhumuni ya kuondoa migogoro, kupanga mipango miji na shughuli nyingine za Serikali lakini pia, ameunda timu mbili za wataalam moja itashughulika na upangaji na upimaji huku ya pili ikishughulika na uhakiki wa wananchi wenye migogoro ambao wanastahili kupewa viwanja mbadala na kazi hiyo itafanyika kwa kipindi cha siku 60 kuanzia sasa ambapo baada ya muda huo, kila mwananchi atafahamu haki yake.

Kadhalika, ametoa onyo kwa viongozi wa Mitaa wenye tabia ya kuuza maeneo kiholela kuacha tabia hiyo mara moja kwani Serikali haitavumilia kuingizwa kwenye migogoro pasi na sababu za msingi ,kwani shughuli hiyo ina wataalam wake ambao ni wa Ardhi lakini pia, ametoa onyo kali kwa watu ambao inasemekana hapo awali walipanga kukwamisha zoezi hilo na kusema kuwa, hatarajii watu hao kuendelea na mipango hiyo kwani Serikali imefikia mwisho kwenye suala hilo.

Eneo la Mahomanyika lilikua na ukubwa wa Hekta 22,000 huku eneo lenye mgogoro likiwa na ukubwa wa hekari 4,363 katika Kata ya Nzuguni, kwa mujibu wa Mpango Kabambe ulioandaliwa mwaka 1979 lilipangwa kuwa ukanda wa kijani lakini baadae Mpango huo ulibadilisha matumizi yake na kuwa mashamba ya mjini, mwaka 2022, Halmashauri ya Jiji ilipanga kumega eneo la ekari 4,393 na kupanga viwanja 9,890 na jumla ya viwanja 2,878 vilipimwa kwa dhumuni la utatuzi wa migogoro ingawa zoezi hilo lilikumbwa na malalamiko kutoka kwa wananchi waliodai ni wamiliki wa asili wa eneo hilo.





## WAZAZI/WALEZI WASISITIZWA KUPELEKA WATOTO KWENYE SHULE ZA AMALI ILI WAPATE UJUZI STAHIKI

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, Februari 26, 2026, amefanya ziara ya kikazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino iliyolenga kutembelea miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na mradi wa shule ya sekondari ya amali Nzali, Kituo cha afya Msanga, Daraja la mawe Mpera Jeshini, ujenzi wa Ofisi ya TANESCO Wilaya ya Chamwino na shamba darasa la kilimo cha Tufaa ambayo inaendelea kutekelezwa kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma na uendelezaji Wananchi kiuchumi.

Akiwa katika shule ya sekondari ya amali Nzali, Mhe. Senyamule amewasisitiza wazazi na walezi kupeleka watoto shuleni hapo ili kupata elimu na ujuzi kwa faida ya kijiji hicho na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla.

"Watoto watakaofaulu kuja katika shule hii asikosekane hata mmoja, fedha zilizotolewa hapa ni nyingi, tumesikia shilingi Bilioni 1 na Milioni mia sita, kazi yake ni kuona watoto wanakuja shuleni ili wapate ujuzi unaostahili, tumeona kuna jengo la TEHAMA la kisasa, mambo ya magari, ufundi wa ujenzi na mambo mengine, tukitumia vizuri, sisi wana Nzali, Chamwino na Dodoma kwa ujumla tutapata vijana wenye ujuzi wa kujenga shule kama hii wenyewe".

Kutokana na mradi huo, Mhe. Senyamule amelipongeza Shirika hilo kwa utekelezaji wa mradi na kuongeza kuwa Serikali kwa sasa ipo kwenye hatua za kupeleka umeme kwenye vitongoji, kutokana na hilo, kuna ongezeko kubwa la wananchi wanaohitaji huduma hiyo maeneo ya vijijini hivyo uwepo wa ofisi hiyo utarahisisha huduma na msaada wa haraka kwao.

Mhe. Senyamule alihitimisha ziara yake katika shamba darasa la kilimo cha Tufaa lililopo eneo la Manchali 'A' linalosimamiwa na kikundi cha BBT 001 Wanyausi kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa maelekezo yake kwa kila Halmashauri kutenga eneo kwa ajili ya kilimo hicho ikiwa ni Mkakati wa Mkoa kuinua wananchi wake kiuchumi kupitia zao hilo ambapo kikundi hicho kilipatiwa miche 420 ambayo mpaka sasa imetimiza miezi miwili na maendeleo yake ni mazuri.






## MKOA WA DODOMA WAINGIA MKATABA NA SHIRIKA LA LYRA IN AFRIKA UJENZI WA MABWENI YA WASICHANA SHULE ZA SEKONDARI

Mkoa wa Dodoma na Shirika la 'LYRA IN AFRICA' lenye Makao makuu yake Mkoani Iringa wamesaini Mkataba wa Mradi wa ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike kwenye shule za sekondari 10 katika Halmashauri tatu za Mkoa wa Dodoma ambazo ni Bahi, Kondoa Mji na Kongwa ambapo lengo lake ni kufikisha elimu ya TEHAMA vijijini ili kuleta uwiano kwa wanafunzi wa Mijini na Vijijini.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo iliyofanyika kwenye Ofisi yake Jengo la Mkapa Jijini humu, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule ambaye ameshuhudia utiaji sahihi huo, amesema kuwa, kupitia Mradi wa ujenzi wa Mabweni hayo, utakwenda kusaidia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa kuinua ufaulu kwa wanafunzi wa Mkoa wa Dodoma ambao umeanza miaka mitatu iliyopita.

"Katika mipango yetu ya kuongeza ufaulu kwenye shule za sekondari ilikua ni kuwafanya watoto wakae 'hostel' kwa hiyo ndio maana mlipokuja mkaona furaha yetu imekua kubwa kwa sababu mmekuja kuungana na juhudi ambazo tayari Mkoa ulianzisha na mipango sasa ni kama ninyi mmekuja kuendeleza zile jitihada tulizozianzisha ambapo tunaamini Hosteli hizi zitasaidia kuongeza ufaulu kama tulivyokua tukitarajia".

Akizungumza wakati wa kutambulisha mradi huo, Mkurugenzi wa Shirika hilo Dkt. Gerald Usike amesema wanatekeleza mradi wa ujenzi wa Mabweni unaokwenda sambamba na kusimika mifumo ya masomo ya TEHAMA kwenye shule hizo kutokana na mradi huo kujenga vyumba kwa ajili ya masomo ya Kompyuta pia wanatoa ufadhili kwa wasichana waweze kujikimu kwa mahitaji mbalimbali pindi wanapokua kwenye mabweni hayo.

Mradi wa ujenzi wa Mabweni, Maabara za TEHAMA, usimikaji wa Mifumo ya Kompyuta sambamba na uwezeshaji kwa wanafunzi wa kike kumudu mahitaji yao pindi watakapoishi kwenye Mabweni, ni muendelezo wa Mradi kama huo ambao ulishawahi kutekelezwa na Shirika hilo kwenye Wilaya ya Chamwino na sasa umerudi tena kwa katika Halmashauri hizo tatu za Bahi, Kondoa Mji na Kongwa.






## WADAU WA BIASHARA WAJENGEWA UWEZO WA KULIFIKIA BARAZA LA USHINDANI (FCT)

Baraza la ushindani (FCT) Mkoa wa Dodoma, Februari 27, 2026, limefanya semina ya kuwajengea uwezo wadau ambao ni wafanyabiashara juu ya uelewa wa namna ya kulifikia baraza hilo ambapo Semina hiyo imefanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Jengo la Mkapa Jijini humu.

Akifungua semina hiyo, Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Bi. Mwajabu Nyamkomora, amebainisha majukumu ya Baraza la Ushindani kuwa ni kutoa maamuzi ya Rufaa zinazotokana na maamuzi yanayotolewa na Taasisi za FCC, EWURA, LATRA, Udhibiti wa Anga (TCAA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Mawasiliano (TCRC) na Mamalaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa nishati ya Petroli (PORA).

Ameongeza kuwa elimu itakayopatikana baada ya semina hiyo, itasaidia kuongeza kasi ya uwajibikaji katika soko na kutatua migogoro ya kiushindani baina ya wadau kwa kuwa ndio jukumu kubwa la Baraza hilo.

Semina hiyo imekwenda sambamba na mawasilisho mbalimbali kama vile Chimbuko la Baraza, Madhumuni, Majukumu, Umuhimu wa Baraza, Mamlaka ya Baraza, Utaratibu wa kuwasilisha Rufaa pamoja na kuwafundisha washiriki utaratibu wa kuwasilisha na kusajili Rufaa kwa njia ya Kielektroniki.

Baraza la Ushindani linaundwa na Mwenyekiti na Wajumbe sita kwa mujibu wa kifungu cha 83(2) cha Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003 ambapo Mwenyekiti na Wajumbe wote huteuliwa na Rais wa Tanzania na hushikilia wadhifa huo kwa kipindi cha miaka mitatu ambapo Mwenyekiti wake ni Jaji wa Mahakama Kuu na Wajumbe ni watu wenye utaalam na uzoefu katika masuala ya kisekta, hususan uchumi, sheria, biashara, viwanda na utawala.





Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma**



# KERO YAKO
## Wajibu Wangu
### Tabasamu na Samia





**Mhe. Rosemary Senyamule**
**Mkuu wa Mkoa wa Dodoma**



**Dkt. Khatibu Kazungu**
**Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma**

*Limetolewa na:*
*Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*
*Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma*

**TUFUATILIE KUPITIA:**
Mkoa wa Dodoma
Dodoma Rs Tv
Jengo la Mkapa, Barabara ya Hospitali

*Pakua jarida hili kupitia website yetu ya: www.dodoma.go.tz*